# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

**MKATABA NAMBA. LGA/180/2021-2022/W/53 LOT 02**
**WA**
**UFUNDI WA UJENZI WA BANDA MOJA SOKO LA MBEZI LUIS**
**(SIZE 20X10M)**

**KATI YA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO S. L. P 55068 DAR ES SALAAM**

**NA**

**FUNDI MWENYEJI – MALEGI JOHN GIBUYI**
**DAR ES SALAAM**



CamScanner

**ATABA WA UFUNDI WA UJENZI WA BANDA MOJA SOKO LA MBEZI LUIS SIZE (20X10M ) KWA KUTUMIA FUNDI MWENYEJI**

Makubaliano haya yanaingiwa leo tarehe.......15..........mwezi .......06.......mwaka.......2022.........

**KATI YA**

**MALEGI JOHN GIBUYI** **ambaye** anafanya shughuli za Ujenzi mkoa wa Dar es Salaam ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Fundi mwenyeji **"LOCAL FUNDI"**:

**NA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO S.L.P 55068 DAR ES SALAAM** ambayo imeanzishwa na Sheria ya Serikali za mitaa (Mamlaka za miji) Sura ya **288** iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 ambaye kwa upande wa pili atajulikana kama **"Mwajiri"**.

**KWAKUWA "Local Fundi"** ana nia ya kufanya kazi ya ujenzi wa banda moja soko la mbezi luis size (20x10m).

**KWAKUWA** "Mwajiri" ana nia ya kukamilisha ujenzi wa banda moja soko la mbezi luis size (20x10m).

**HIVYO BASI**, mkataba huu unashuhudia yafuatayo:-

**MASHARTI YA MKATABA**

1. Kwamba mkataba huu ni wa muda wa ......WIKI 6......na unaanza kutumika tarehe ....15/06/2022.....hadi ....26/07/2022....

   Kwamba mkataba wa Ujenzi banda moja soko la mbezi luis size (20x10m).
2. utatekelezwa kwa mchanganuo ufuatao katika jedwali hili:-

**JEDWALI NA. 1 MAELEZO YA KAZI NA GHARAMA BANDA MOJA SOKO LA MBEZI LUIS SIZE (20X10M )**

| NA. | AINA YA KAZI | BEI (TSHS) | MAKATO 5% | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kuset na kuchimba msingi | 700,000.00 | 35,000.00 | 665,000.00 |
| 2. | Kuset vitako vya nguzo na kumimina zege | 500,000.00 | 25,000.00 | 475,000.00 |
| 3. | Kusuka nondo za vitako na nguzo za msingi | 200,000.00 | 10,000.00 | 190.000.00 |
| 4. | Kujenga tofali za msingi | 700,000.00 | 35,000.00 | 665,000.00 |
| 5. | Kusuka mbao za boksi na nondo(Nguzo wima na Mlalo) | 500,000.00 | 25,000.00 | 475,000.00 |



CamScanner

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kujaza kifusi,kushindilia na kupanga mawe | 500,000.00 | 25,000.00 | 475,000.00 |
| 7. | Kutandika DPM na kumwaga zege jamvi,nguzo mlalo na wima | 1,000,000.00 | 50,000.00 | 950,000.00 |
| 8. | Kujenga ngazi na Ramp za jengo kwa maelekezo ya msimamizi | 200,000,00 | 10,000.00 | 190,000.00 |
| 9. | Kuchomea bolt na nguzo | 300,000.00 | 15,000.00 | 285,000.00 |
| 10. | Kukata plate na kutoboa na kuzichomea na nguzo | 1,000,000.00 | 50,000.00 | 950,000.00 |
| 11. | Kusimamisha nguzo kwa bolt | 400,000.00 | 20,000.00 | 380,000.00 |
| 12. | Kuunda kenchi na kupaua pamoja na kufunga bati za kivuli kenchi ya mbele na nyuma | 2,900,000.00 | 145,000.00 | 275,5000.00 |
| 13. | Kupaka rangi banda | 250,000.00 | 12,500.00 | 237,500.00 |
| 14. | Kufunga mfumo wa umeme (FIRST FIXED AND SECOND) | 400,000.00 | 20,000.00 | 380,000.00 |
| **JUMLA TSHS** | | **9,550,000.00** | **477,500.00** | **9,072,500.00** |

3. Kwamba pande zote zimekubaliana kuwa Fundi Mwenyeji atalipwa malipo yake kwa awamu tano(14) zenye jumla ya **Tshs 9,550,000.00 (Shilingi Milioni Tisa laki tano na hamsini elfu tu. )** ikiwa ni malipo kwa kazi zote kama inavyoonekana katika **jedwali Na. 1**

4. Malipo yatafanyika baada ya kupima na kukagua kazi kwa kila awamu na pande mbili zitashirikiana.

5. Kwamba fundi Mwenyeji atafanya kazi yake kwa uaminifu mkubwa.

6. Kwamba fundi Mwenyeji atawajibika kulipa au kurudisha kazi iwapo ataharibu kazi aliyopewa kulingana na mahitaji aliyoyaomba.

7. Kwamba msimamizi wa mradi ni Kamati ya ujenzi ya Kituo cha Ukusanyaji Mapato Manzese na watahakikisha kazi inafanyika kwa mujibu wa mkataba kwa kuzingatia maelekezo ya Mhandisi wa Manispaa.

8. Kwamba Fundi Mwenyeji atalipwa malipo yake yote ya awamu tano (05) ikiwa ni pamoja na makato yote (retantion money) baada ya ukamilishaji wa ujenzi wa Kontena katika Kituo cha ukusanyaji mapato cha Manzese makato hayo yana jumla ya **Tsh. 477,500.00 (Shilingi laki nne sabini na saba elfu na mia tano tu ).**

9. Kwamba Mhandisi wa Manispaa atakagua kazi kabla ya kuidhinishiwa malipo na kwamba ni jukumu la Mhandisi wa Manispaa kuhakikisha kuwa kazi inakidhi ubora wa kitaalamu.

10. Kwamba Fundi Mwenyeji akishindwa kutimiza masharti ya mkataba huu, mkataba utavunjwa.

11. Kwamba baada ya mkataba kuvunjwa, malipo yatafanyika kwa kiwango cha kazi iliyofanyika baada ya tathmini ya Mhandisi wa Manispaa kufanyika.

12. Kwamba pande zote mbili zitatakiwa kutoa tarifa iwapo upande wowote hauridhiki na kazi ili hatua zichukuliwe.

13. Kwamba upande wowote unaweza kuvunja mkataba kwa kutoa Ilani ya maandishi ya muda wa ……………………ya kuvunja mkataba.

14. Kwamba mkataba huu unasimamiwa na sheria za Tanzania

**KUKAMILISHA MAKUBALIANO**

| | |
|---|---|
| **MWAJIRI**<br>**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**<br>**S.L.P 55068**<br>**DAR ES SALAAM** | **MWANASHERIA**<br>**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**<br>**S.L.P 55068**<br>**DAR ES SALAAM** |
| **SAINI:** ……[signature]……<br>**JINA: BEATRICE DOMINIC**<br>**TAREHE:** …20/06/2022…<br>**ANWANI:** 55068 S.L.P, DAR ES SALAAM<br>**CHEO:** MKURUGENZI WA MANISPAA<br>**MUHURI WA OFISI**<br>MKURUGENZI WA MANISPAA<br>HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO<br>DAR-ES-SALAAM | **SAINI:** …[signature]…<br>**JINA:** …FORTUNATA SHEM…<br>**TAREHE:** …17/06/2022…<br>**ANWANI: DAR ES SALAAM**<br>**CHEO** ………MWANASHERIA WA MANISPAA YA UBUNGO<br>HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO<br>**MUHURI/DOLE GUMBA:** S. L. P. 55068<br>DAR-ES-SALAAM |
| **FUNDI MWENYEJI: MALEGI JOHN GIBUYI** | **SHAHIDI** |
| **SAINI:** …[signature]…<br>**JINA:** …MALEGI JOHN GIBUYI<br>**TAREHE:** …17/06/2022…<br>**ANWANI:** …S.L.P 76114 DSM<br>**CHEO:** …FUNDI…<br>**MUHURI:** | **SAINI:** …[signature]…<br>**JINA:** …OMARY SAID…<br>**TAREHE:** …17/06/2022…<br>**ANWANI:** S. L. 55068, **DAR ES SALAAM**<br>**CHEO:** …FUNDI…<br>**MUHURI:** |



CamScanner